

JIMBO KATOLIKI IRINGA

TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI TOSAMAGANGA (TIHAS)



S.L.P 50 Tosamaganga
IRINGA

SIMU: 0769 432 532 (MKUU WA TAASISI)/ 0762 482 704 (MHASIBU)/0744 666 633
BARUA PEPE: tosamagangainstitute@gmail.com TOVUTI: www.tihhas.ac.tz

YAH: WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO KOZI YA UTABIBU, UUGUZI NA UKUNGA NA UPGRADING MWAKA MMOJA

UTANGULIZI

Tunayofuraha kukuaribisha hatika Tasisi yetu ya Afya na Sayansi Shirikishi Tosamaganga. Chuo chetu kinatoa kozi mbili za afya ambazo ni Utabibu (Clinical Medicine) na Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifery)

MAHALI TAASISI ILIPO

Taasisi ipo Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Iringa Vijijini eneo la Tosamaganga ikiwa ni kilomita 15 kutoka Iringa mjini. Kutoka mjini unapanda daladala zinazoanzia **Stendi kuu ya zamani** zilizoandikwa **Iringa Mjini / K.Kilolo-Ipamba - Tosamaganga**. Unashukia kituo cha hospitali Teule ya Wilaya Tosamaganga. Chuo kimo ndani ya geti la hospitali ambayo wanafuzi wetu hutumia kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

GHARAMA ZA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UUGUZI NA UKUNGA (ORDINARY DIPLOMA IN NURSING AND MIDWIFERY), UTABIBU (CLINICAL MEDICINE) NA KOZI YA UUGUZI NA UKUNGA YA MWAKA MMOJA (UPGRADING NURSING)

ADA NA MALIPO MENGINE KWA UTABIBU (CLINICAL MEDICINE) 2022-2023

Na	AWAMU	ADA	MALAZI (Hostel)
1	Awamu ya kwanza (Wakati wa kuripoti muhula wa kwanza)	550,000	BURE
2	Awamu ya pili (mwezi Februari)	550,000	BURE
3	Awamu ya tatu (Wakati wa kuripoti muhula wa pili)	550,000	BURE
4	Awamu ya nne (Mwezi Julai)	550,000	BURE
	JUMLA	2,200,000/=	BURE

ADA NA MALIPO MENGINE KWA UUGUZI NA UKUGGA (NURSING AND MIDWIFERY) 2022-2023

Na	AWAMU	ADA	MALAZI (Hostel)
1	Awamu ya kwanza (Wakati wa kuripoti muhula wa kwanza)	500,000	BURE
2	Awamu ya pili (mwezi Februari)	500,000	BURE
3	Awamu ya tatu (Wakati wa kuripoti muhula wa pili)	500,000	BURE
4	Awamu ya nne (Mwezi Julai)	500,000	BURE
	JUMLA	2,000,000/=	BURE

ADA NA MALIPO MENGINE KWA UUGUZI NA UKUNGA MWAKA MMOJA (UPGRADING) 2022-2023

Na	AWAMU	ADA
1	Awamu ya kwanza (Wakati wa kuripoti muhula wa kwanza)	450,000
2	Awamu ya pili (mwezi Februari)	450,000
3	Awamu ya tatu (Wakati wa kuripoti muhula wa pili)	450,000
4	Awamu ya nne (Mwezi Julai)	450,000
	JUMLA	1,800,000/=

NB: Wanafunzi wa in-service wanajitegemea kwenye upande wa malazi

NAMNA YA KULIPA

Kwa awamu ya kwanza gharama za Ada iliyoainishwa kwenye jedwali ilipwe kwenye akaunti ya Taasisi ambayo ni 0150579891200 – CRDB Jina la akaunti ni “TOSAMAGANGA INSTITUTE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES”. Baada ya kuripoti mwanafunzi atapewa CONTROL NUMBER ya malipo ya ADA ambapo atakua akilipia awamu zinazofuata.

MALIPO MENGINE KULIPWA KWA TASLIM (CASH) AMBAYO NI;

1. Gharama ya mitihani ya taifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni **Tshs.150,000/=**
2. Ada ya Udhhibiti Ubora (Quality Assurance Fee) Tshs.15,000/= Kwa ajili ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi **(NACTE)**,
3. Matibabu **Tshs.52,400/=** kwa asiye na bima na kwa mwenye bima afike na bima yake **(UJE NA FEDHA MKONONI)**
4. Sare ya Taasisi – **Tshs.120,000/=**
5. Gharama za udhibiti ubora (Quality Assurance) - **Tshs.15,000/=**
6. Serikali ya wanafunzi - **Tshs.10,000/=**

NB:

1. Ada haitabadilika katikati/ndani ya mwaka wa masomo, lakini inaweza kubadilika mwanzo wa mwaka wa masomo unaofuata kutegemeana na mabadiliko ya uchumi wa Taasisi, Jimbo na Nchi.
2. Wale tu ambao wamelipa nusu ya ada ya muhula ndio watakasajiliwa kwenye muhula husika.
3. Ada ikishalipwa hairudishwi.
4. Ada unaweza kulipa yote au kwa awamu nne kama ilivyoainisha kwenye jedwali
5. Mwanafunzi asipotimiza kulipa ada kwa awamu husika hatapokelewa au atarudishwa nyumbani na akikaa nyumbani kwa muda wa siku 20 na zaidi atapaswa kurudia mwaka
6. Gharama za marudio ya mtihani (supplementary exam) ni Tsh. 50,000/= kwa somo na maombi ya mtihani maalumu (Special sit exam) ni Tsh. 50,000 kwa kila somo

MUHIMU

MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NA VIFAA / MAHITAJI YAFATAVYO

Vifaa vya matumizi binafsi

- a. Mashuka manne- pink (ke), bluu(me)
- b. Neti ya kujikinga na mbu
- c. Blanketi
- d. Vifaa vya michezo; track suit nyeusi
- e. Nguo ya kulalia usiku, mto na taulo
- f. Godoro dogo 2.5*6, Taasisi kitatoa kitanda.
- g. Viatu vya ngozi, vyeusi (**VISIVYO KUWA RABA**)
- h. Kijiko, kikombe cha chai, ndoo kubwa (plastic), dishi, bakuli na sahani
- i. Sweta rangi ya nyeupe.

Vifaa vya mazoezi kwa vitendo

- a. Saa ya kifuani
- b. BP-MACHINE -Aneroid
- c. Stethoscope standard (Economy model)
- d. Mercury thermometer
- e. Tape measure
- f. Penlight
- g. Patella hammer
- h. Stop watch
- i. Torch

Tunakutakia maandalizi mema na KARIBU.
ASANTE!!